JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKODARI KISARIKA,
S.L.P 454,
MOSHI.
TEL.No: +255 754201379/0787201379
11/05/2018

KUMB NA.KSS/FV/2018/2019
JINA LA MWANAFUNZI……
S.L.P……..
……...

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO
KISARIKA SEKONDARI MWAKA 2018/2019

1.0. Ninayo furaha kubwa kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii, Mchepuo wa Sayansi – chaguo (Combination) la ……..

Shule iko Wilaya ya Moshi vijijini, Umbali wa km 11 kutoka stend kuu ya Mabasi ya Moshi Mjini. Usafiri wa kufika shuleni unapatikana stend kuu ya Moshi mjini, na utapanda magari yaendayo Uru Mawela na utashuka Kituo cha **K.N.C.U au Timbirini**. Tarafa ya Hai mashariki, Kata ya Uru Kaskazini katika kijiji cha Ongoma – kitongoji cha Manoshi.Shule ni ya mchepuo wa Kilimo.

Tafadhali soma kwa makini sana maagizo yafuatayo na ukamilishe Mahitaji yote yaliyopo kwenye barua hii ili uweze kupokelewa shuleni na kuanza masomo bila usumbufu wowote.

2.0. Shule itafunguliwa tarehe **02/07/2018**, tafadhali fika tarehe hiyo bila kukosa ukiwa na vitu vifuatavyo ili uweze kuandikishwa shule. Mwisho wa kuripoti shuleni ni Tarehe **15/07/2018;**

i) Cheti cha Daktari kinachoonesha kuwa umepimwa vizuri kwenye Hospitali ya Serikali iliyoko karibu nawe (Fomu No.1 imeambatanishwa)

ii) Fomu No.2, ya kukubali/Kutokukubali nafasi ya Kidato cha Tano Mwaka 2018/2019 Kisarika Sekondari, na maelezo ya mzazi kukiri na kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

iii) Fomu No.3, ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na kujiandikisha shuleni.

iv) Fomu No 4, ya Utii wa Sheria na Tabia njema/mkataba wa kutokushiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai.

(v) Form Four Result slip

(vi) Leaving certificate ya Form IV na cheti cha kuzaliwa (vii) Picha 4 za rangi (kivuli cha bluu akiwa amevaa sare ya shule.)

Kama mwanafunzi ana kitambulisho cha Bima ya afya kitakuwa msaada mkubwa kwake kwa ajili ya matibabu hivyo akumbuke kuja nacho.

2.1. ADA NA MICHANGO MINGINE YA SHULE.

S/N	MAELEZO YA MALIPO	MUHULA WA I	MUHULA WA II	JUMLA KWA MWAKA
1.	Karo ya shule	35,000	35,000	70,000
2.	Tahadhari	10,000	-	10,000
3.	Kitambulisho & Picha	6,000	-	6,000
4.	Uboreshaij wa Taaluma	10,000	10,000	20,000
5.	Ulinzi & wapishi	15,000	15,000	30,000
6.	Nembo ya shule	2,000	-	2,000
7.	Dawati	15,000	-	15,000
8.	Ukarabati	15,000	-	25,000
9.	Huduma ya kwanza	5,000	5,000	10,000
	JUMLA KUU	**123,000**	**65,000**	**188,000**

N/B:

MALIPO YOTE YA SHULE YALIPWE KWA PAMOJA KWENYE A/C YA SHULE N0. 40301000159 ILIYOPO NMB, KUANDIKA JINA LA MWANAFUNZI NA KIDATO ANACHOSOMA, KISHA KUWASILISHA BANK PAY – IN SLIP SHULENI SIKU UNAPORIPOTI SHULENI: KAMA UTALIPA SHULENI, MALIPO YAKO YATAKUWA NI BATILI.

2.2.SARE ZA SHULE

2. **Mwanafunzi ajinunulie mwenyewe sare zifuatazo:-**

A) SARE ZA DARASANI

Sare za shule hii ni Suruali 2, rangi ya light blue, yenye upana wa kutosha, isiyobana mwili, yenye rinda 2 kwa mbele, mfuko mmoja wa nyuma wa kufunga na kifungo siyo kwa zipu na iwe na pindo la chini (Turn up),Sweta 1 light blue, shati 2 nyeupe za mikono mirefu, tai moja rangi ya light blue(tetron material),Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili vyenye kamba vinavyofunika miguu na visiwe na visigino virefu.,Soksi jozi mbili nyeusi na mkanda mweusi wa ngozi.

Mwanafunzi ajinunulie mwenyewe sare hizo isipokuwa T-shirt 1 yenye nembo ya shule (Itapatikana shuleni kwa gharama ya Tshs 10,000/=)

B: SARE ZA KUSHINDIA ANAPOKUWA NJE YA DARASA

Mwanafunzi awapo shuleni ataruhusiwa kuvaa mavazi rasmi yaliyoainishwa hapa chini, na hataruhusiwa kuvaa mavazi (nguo) mengine tofauti na hayo. Atakayevaa mavazi tofauti na hayo atanyang'anywa na yatapatiwa wale wasiojiweza na wanaoishi katika mazingira magumu. Hivyo nunua (i) Suruali nyeusi za kitambaa 2.(Sio jeans) zilizoshonwa vizuri. (2) T-shirt 2 za njano (plain) zisizokuwa na maandishi na zenye shingo ya (round neck) (3) Bukta ya njano na raba za michezo. (4) Nunua jacketi zito kwa ajili ya kuvaa usiku wakati wa preparation lenye rangi moja na lisiwe na maandishi yoyote.

NB: Mwanafunzi hataruhusiwa kuvaa nguo za nyumbani na wala asije nazo kabisa.

Aidha wanafunzi Hawaruhusiwi kuja na vitu vilivyoorodheshwa hapa chini. Mwanafunzi akionekana navyo ataadhibiwa vikali na vitu hivyo vitachukuliwa na hawatarudishiwa.

(a) Simu ya mkononi (ASIJE NAYO **KABISA** shuleni) pamoja na;
(b) Radio au Radio Cassete.
(c) Pasi ya Umeme
(d) "Heater"
(e) Kamera
(f) Vyakula vya aina yoyote
(g) Vileo vya aina yoyote
(h) Nguo binafsi na viatu mbali na sare ya shule.
(i) Vidani (mkufu, pete, shanga.n.k.

2.3: MAHITAJI MENGINE MUHIMU

1:1 VITABU.

Ni wajibu wa mzazi/mlezi kuhakikisha kuwa mwanafunzi anakuwa na uwezo wa kujinunulia vifaa muhimu vya masomo hasa vitabu kwani Shule haijawa na vitabu vya kutosheleza kwa kila mwanafunzi. Tunategemea kununua kulingana na upatikanaji wa fedha.Vitabu vichache vinavyopatikana wataazimishwa.Mwanafunzi atakayeazimishwa kitabu asiporudisha anapotakiwa kufanya hivyo atahesabiwa kuwa na kosa la kutorudisha mali ya shule na hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake ikiwa ni pamoja na kunun ua kitabu kipya. Upotevu wa kitabu utafidiwa kwa kutoa kitabu kingine cha aina hiyo wala si fedha. Orodha ya vitabu vya F 5/6 kwa kila somo ni kama ilivyoanishwa hapa chini.

GEOGRAPHY PAPER I.

1. Principles of physical Geography – by F.J. Monk house
2. A comprehensive Approach to Physical Geography for secondary School – by D.T. Msabila.
3. Practicle Geography for Africa – by John M. Prichard.
4. Land forms 1 Africa – An Introduction to Geomorphology – by Colin Buckle.
5. Africa – by J.M. Prichard.
6. Geography, An Integrated Approach by David Waugh.
7. Physical geography By Charles Plummer
8. Foundation of physical geography By B. Michael.

GEOGRAPHY PAPER II.

1. Human and Economic Geography – by Goh cheng & Morgan.
2. Advanced level Geography cource book – by Tanzania Institute of Education (TIE)
3. An Integrated Focal Regional study on Human and Economic Geography Advanced level paper 2 – by D.T. Msabila.

PHYSICS BOOKS:

1. Nelkon and Parker
2. Understanding Physics.
3. Rodger Manchester.
4. Calculation for A-level

MATHEMATICS.

1. Pure Mathematics Vol. 1

CHEMISTRY REFERENCE BOOKS.

1. Freementle M. Chemistry in Action. Macmillan Education Ltd. 3rd Education.
2. Mzumbe Book Project. Physical chemistry.
3. Advanced Chemistry – Ann & Patrick.
4. Ramsden E.N. (A level chemistry
5. Chemistry (Raymond Chang)
6. University chemistry

TEXT BOOKS (BIOLOGY).

1. Taylor D. Green N. & Stout G. Biological Science (3rd Edition.
2. Roberts M.B. (1986). New understanding Biology (4th Edition).
4. S.O. Loeje – Certificate Practical Biology.

1:2. VIFAA VINGINE VYA MASOMO

1. Calculators kidato cha 5 na 6.(Scientific calculator).
2. Daftari kubwa 15.
3. Mathematical set, kalamu za wino, risasi, rula n.k
4. Vitabu vya ibada kwa mujibu wa madhehebu/ dini yako.
5. Lab coat nyeupe.

9. Ni muhimu ieleweke kuwa mitihani ifuatayo hulipiwa na watahiniwa wenyewe. Mtihani wa Taifa, Mtihani wa mock na Pre-national kwa wanafunzi wa kidato cha sita.

1:3 VIFAA VYA MABWENI.

Uje na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya mahitaji ya bwenini.

1. Godoro la sponji "2½×6"×
2. Shuka mbili rangi ya pinki
3. Blankenti moja
4. Taulo, mswaki, dawa ya meno na malapa.
5. Mto mmoja
6. Chandarua cha mbu
7. Night dress
8. Vyombo vya kulia kama bakuli, sahani, kikombe cha chai na kijiko.

3. FEDHA ZA MATUMIZI (POCKET MONEY).

Mzazi anaweza kumpa mwanafunzi kiasi cha kuridhisha, lakini fedha zitunzwe benki(account yake) ili kuondoa vishawishi vya wizi.

Kila mwanafunzi anayejiunga na shule ya Sekondari Kisarika,anatakiwa kuleta vifaa vifuatavyo siku anaporipoti ili aweze kusajiliwa.

i) Jembe lenye mpini

ii) Ndoo ya maji

iii) Fagio 2 za chelewa zenye mpini unaomwezesha mwanafunzi kufagia akiwa amesimama

iv) Reki ya kukusanyia Taka ngumu 1(Yenye mpini wa chuma)

(v) Ream paper bunda 2, A4 size aina yoyote isipokuwa **Dolfin** Haitapokelewa.kwa ajili ya mitihani na mazoezi (weekly tests)

(vi) Hard broon 1

(vii) Mopar 1

(viii) Dissecting kit – wanaosoma Biology.

(ix). Graph pad moja (1 cm x 1 cm squares of 10 mm x 10mm)

3. <u>SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.</u>

A.Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978.Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu Nchini.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na Nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

1. Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote ,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima,**AMBAPO MWANAFUNZI ANAHITAJIWA**:-

-Kuheshimu picha za viongozi,Nembo ya Taifa,Bendera ya Taifa na Fedha za Taifa.

-Asimame kwa unyenyekevu na kumsalimia yeyote anayemzidi umri mahali popote alipo.

-Asimame kwa unyenyekevu katika mstari au wakati wowote anapopatiwa huduma.

-Anyooshe mkono juu anapojibu au kuuliza swali darasani.

-Kuheshimu ukumbi wa mikutano,Ofisi zote za serikali na majengo yote ya umma.

-Ashirikiane na jamii nzima katika kazi na shughuli zote za ujenzi wa taifa

2.Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni lazima ikiwa ni pamoja na:- Kuzingatia siku za kufungua na kufunga shule,lazima kila mwanafunzi afike kuanza muhula siku iliyopangwa na asiondoke kwenda likizo kabla ya siku kufunga shule. Mwanafunzi yeyote atakayechewa kurudi shuleni kwa muda wa siku 1-3 atalazimika kuleta barua ya mzazi iliyopitishwa na Afisa elimu wa Mkoa au Wilaya anakotoka. Akichelewa kurudi shule kwa kati ya siku tatu mpaka wiki mbili au zaidi atalazimika kufika na mzazi/Mlezi anayetambulika shuleni vinginevyo hatapokelewa.

- Ni lazima mwanafunzi kuwahi shuleni muda uliopangwa na kushiriki katika shughuli zote za shule kama kuitwa majina “Roll calls”, usafi wa mazingira, shughuli za uzalishaji mali, n.k. Atakayechewa au kutokuhudhuria katika shughuli hizo ataadhibiwa kwa mujibu wa sheria.

- Kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa pamoja na michezo Utoro hautegemewi hapa shuleni, endapo mwanafunzi atabainika kuwa mtoro atahesabiwa kutopenda shule na adhabu kali zitatolewa kwa yeyote anayekiuka agizo hili ikiwa ni pamoja na kuiarifu Bodi ya Shule kwa uamuzi zaidi. Ruhusa ya kukosekana katika shughuli yoyote kwa sababu maalum itatolewa na Mwalimu wa zamu kwa kibali maalum.

- Kuhudhuria mikutano yote ya shule kama Baraza la shule, ukaguzi wa usafi n.k.

-Kupandishwa Bendera ya Taifa, Vikao vya madarasa n.k:

-Kutokutoka Darasani bila ya Ruhusa au kibali cha mwalimu.

3.Lugha rasmi ya shuleni ni KIINGEREZA TU (NDANI NA NJE YA DARASA):-Hivyo, mwanafunzi anapaswa kujifunza kwa bidii matumizi sahihi ya lugha hii kwa kusoma,kuandika na kusikiliza.

-Mwanafunzi asitumie lugha chafu ya matusi kwa mtu yeyote.

4. Mwanafunzi anahitajiwa:-
-Awe balozi mzuri wa mazingira ya shule kwa kuyatunza na kuyaboresha wakati wote.
-Avae sare rasmi ya shule wakati wote akiwa shuleni na anaporudi nyumbani.
-Asivae mavazi ya aibu yatakayomdhalilisha yeye, shule na jamii nzima ya Kitanzania.
-Asifuge ndevu, kucha ndefu, nywele ndefu zenye kuwekwa dawa wala kunyolewa kipara.
-Kutembea zaidi ya mmoja wakati wa kuja shuleni na wakati wa kurudi nyumbani.
-Asitembelee bila kibali maeneo yafuatayo: Ofisi ya Mkuu wa Shule,Chumba cha walimu(Staff room),Ofisi zote za shule,Maabara,Jikoni,na Nyumba za Watumishi wa Shule.
-**Ajiepushe kutembelea vilabu vya pombe, majumba ya starehe na nyumba zakulala wageni"Guest Houses".**
5. Mwanafunzi yeyote haruhusiwi kutoa taarifa potofu na isiyo sahihi ndani na nje ya mipaka ya shule.

ADHABU ZENYE MAONYO

Mwanafunzi atakayevunja sheria za shule hapo juu, atachukuliwa hatua zifuatazo;
1. Ataonywa nakupewa adhabu kali na barua kupelekwa kwa mzazi/mlezi wake.
2. Akirudia kuvunja sheria za shule, mwanafunzi atasimamishwa shule kisha mzazi/mlezi wake ataitwa shuleni kumwonya mwanaye,kisha atapewa adhabu kali zaidi kabla ya kuruhusiwa kuendelea na masomo.
3. Akionekana mwanafunzi huyu haonyeki na Taifa linapoteza muda wake na fedha kumuelimisha **ATAFUKUZWA SHULE MOJA KWA MOJA**

B: MAKOSA YENYE KUFUKUZWA SHULE BILA ONYO:-

1. wizi
2. kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/ utoro
3. kugoma na kuhamasisha mgomo
4. kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla
5. kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote Yule
6. kusuka nywele kwa mitindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nyele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule
7. kufuga ndevu
8. ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
9. uvutaji wa sigara
10. uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa
11. kupata ujauzito au kutoa mimba
12. kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
13. kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
14. kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
15. kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
16. kudharau Bendera ya Taifa
17. kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
18. uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

Kama **HUKUBALIANI NA MASHARTI YALIYOTAJWA** katika barua hii ya kujiunga na shule, tafadhali usije shuleni bali mzazi/mlezi akutafutie shule nyingine.

KARIBU SANA KISARIKA SEKONDARI

M.E SAIWA
MKUU WA SHULE.

PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
KISARIKA SECONDARY SCHOOL

FORM No.1.
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

From THE HEADMASTER,
KISARIKA SECONDARY SCHOOL,
P.O BOX 454,
MOSHI.

TEL.No: +255 732 973 666/0787201379

TO: Medical office
……
……
……
Pupil's Name……Age……
Please examine the above named pupil as to fitness for further studies in this school.
1. Aids Test……
2. Blood count (Red & white)……
3. Urinal analysis……
4. Stool analysis……
5. Syphilis Test……..
6. T.B Test……
7. Ear test……..
8. Eye Test……
9. Spleen…….
10. Abdomen……
11. Check cases of pregnancy for girls……..
12. Additional information of any other Physical & mental impairments, hereditary or infectious disease……
……
Treatment after Examination…….
……
……

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by Medical Officer)
I have examined the above mentioned pupil and recommend her/him physically & mentally fit for appointment and re-engagement as above.

Date……..Signature…….

Station……Designation……

FOMU No. 2.
KUKUBALI/KUTOKUKUBALI NAFASI YA KIDATO CHA V MWAKA 2018/2019 KISARIKA SEKONDARI

Fomu hii ijazwe na mzazi/mlezi pamoja na mwanafunzi aliyechaguliwa kuingia kidato cha Tano 2018/2019 kisha mwanafunzi ailete shuleni.

1. Mimi……kwa hiari yangu nimekubali/sikubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na kidato cha Tano katika shule ya sekondari Kisarika.Nitakuwa tayari kuzingatia sheria zote za shule wakati wote niwapo shuleni.Kuvunja sheria ya shule kwa makusudi nitakuwa nimekiuka ahadi hii ninayoitoa na ninastahili kuchukuliwa hatua kali za kinidhamu zinazostahili kosa langu.
2. Na pia nitasoma kwa bidii bila kutegemea nyenzo au mbinu mbadala kama kuibia mtihani ili nifaulu.

Saini ya mwanafunzi…….Tarehe……

BANDIKA
PICHA YA
MWANAFUNZI
HAPA

3.Mimi……Mzazi/Mlezi wa…….
naikubali/siikubali nafasi aliyopewa mwanangu na kwamba muda wote awapo shuleni na popote analazimika kufuata sheria za shule na kuwa mtiifu kwa walezi wake mpaka atakapohitimu masomo yake na kupata ajira stahili.Na kwamba baada ya kukubali hivyo, sitacheleweshe kwa namna yoyote malipo na michango yote iliyotajwa.Natambua kuwa ninao wajibu wa kumlipia ada na mahitaji mengine muhimu.Nikishindwa kufanya hivyo mwanangu arudishwe nyumbani kuchukua malipo hayo kwa gharama zangu.

BANDIKA
PICHA YA
MZAZI/MLEZI
HAPA

4.Nimezisoma kwa makini sheria za shule hii,nimezielewa na kuzikubali.Naahidi kushirikiana na utawala wa shule kwa kuhakikisha kuwa mwanangu anazielewa,anazikubali na kuzifuata kwa dhati kwa muda wote atakapokuwa shuleni.Nakubali kuwa mwanangu akishindwa au akikataa kutii sheria hizo na asipojirudi baada ya kuonywa na walimu na walezi wake arudishwe nyumbani mara moja.

Jina la mzazi/mlezi……Saini…….Tarehe……..

FOMU Na.3.

KUJIANDIKISHA SHULE.

A: HABARI ZA MWANAFUNZI.

1.Jina kamili(kama kwenye mtihani)……..
2.Tarehe ya kuzaliwa……..Dini…….
3.Mahali na wilaya ulikozaliwa……..
4.Shule uliyomalizia Darasa la saba ……kidato cha nne……
5.Masomo unayopendelea
(i)……(ii)……(iii)……(iv)……(v)……(vi)…….....(vii)……
……
6. Kazi yoyote ya uongozi uliyowahi kufanya kama vile kiongozi wa michezo,kwaya,ngoma,kiranja,maktaba n.k.
7. Mambo unayopendelea kufanya nje ya masomo kama michezo,ushonaji n.k.
i)……..ii)……iii)……
8. Ninathibitisha kwamba habari/taarifa nilizozitoa hapo juu ni za kweli na ni sahihi.
Saini ya mwanafunzi ……..Tarehe……

B. HABARI ZA MZAZI/MLEZI.

1. Jina kamili la baba……yuko hai/mfu.
2. Kazi yake……
3. Jina kamili la mama ……..yuko hai/mfu.
4. Kazi yake……
5. Jina kamili la mlezi (iwapo mwanafunzi haishi na wazazi wake)…….
6. Kazi ya mlezi……
7. Nambari ya simu ya mzazi/mlezi……
8. Anuani ya mzazi/mlezi……
9.Mwanafunzi anaishi na:-(i)Baba tu (ii)Mama tu(iii)Wazazi wote (iv)Mlezi (*Kata isiyohusika **)**
10. Taja ndugu sita wa karibu wanaoruhusiwa kumsaidia/kumtembelea mwanafunzi awapo shuleni.

S/N	JINA	SIMU Na.	ANUANI	UHUSIANO
1				
2				
3				
4				
5				
6				

11. Mimi…….ambaye ni baba/mama/mlezi wa……
Nathibitisha kuwa taarifa hiyo hapo juu ni sahihi na ninaahidi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia njema/nzuri, mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo.
Jina na Saini ya mzazi/mlezi……Tarehe……

FOMU Na.4.

UTII WA SHERIA NA TABIA NJEMA.

Mimi……(Jina kamili) wa kidato cha Tano 2016/2017 natambua wajibu wangu kwa Taifa kama mwanafunzi na ninaahidi:-

1).Kwamba Nitatii na kuwaheshimu Viongozi wangu wote kuanzia ngazi ya Monita, Viranja, Walimu, Watumishi wote hadi Mkuu wa Shule.

2).Kwamba nimezisoma na kuzielewa na nitazifuata sheria na kanuni za shule pamoja na maelekezo yote yatakayotolewa mara kwa mara na uongozi wa shule.

3). Kwamba sitashiriki katika migomo yoyote, fujo na makosa yote ya jinai.

4).Kwamba sitatoka nje ya mipaka ya shule wakati wote wa masomo labda tu kwa shughuli maalumu na baada ya kupata kibali kutoka nje kutoka kwa mwalimu au mkuu wa shule mwenyewe.

5).Kwamba kama nitashindwa kufuata hayo yote hapo juu,hatua kali zichukuliwe dhidi yangu ambazo ni pamoja na kusimamishwa shule ama kufukuzwa shule.

Jina na Saini ya mwanafunnzi……Tarehe……

Jina na Saini ya Shahidi mzazi/mlezi……Tarehe……

Saini ya Mkuu wa Shule……Tarehe……